

LIPA KODI YA ARDHI KILA MWAKA

Kodi ya pango la ardhi

1. Kodi ya Ardhi ni nini?

Kodi ya ardhi ni malipo ya pango la ardhi wanayotozwa wamiliki wa viwanja na mshamba yaliyopimwa na kumilikishwa kisheria

2. Kwa nini kodi inalipwa?

1.Ni kutimiza masharti/mkataba unaomtaka Mmiliki kulipia kodi ya pango la ardhi kila mwaka tarehe 1 (Mosi) Julai.

2.Unalipa kwa kunufaika na matumizi ya ardhi hiyo kwa kipindi ulichopewa.



3. Nani anatakiwa kulipa kodi hiyo?

Mtu yeyote anayemiliki ardhi ili-yopimwa kisheria iwe imeendelezwa au haijaendelezwa anapaswa kulipa kodi ya pango

4. Misingi ya ukadiriaji wa kodi ya ardhi ni ipi?

- Ukubwa wa ardhi inayomilikiwa
- Thamani ya ardhi mahali ilipo (land value)

•H u d u m a m u h i m u zilizopo(miundombinu)

•Matumizi ya ardhi husika kama vile Biashara, viwanda, makazi, kilimo, ibada n.k

5. Makadirio na malipo ya kodi ya ardhi yanafanyika wapi?

Kwa wamiliki wa ardhi Dar es Salaam, makadirio na malipo ya kodi yanafanyika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kivukoni kwenye Kitengo cha Kodi na katika Ofisi za Ardhi za Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke.Kwa mikoani, makadirio hufanywa kwenye Ofisi za Ardhi zinazotambulika za Manispaa na Halmashauri za Miji na Wilaya.

6. Ni zipi athari za kufanyiwa makadirio nje ya maeneo hayo?

- Kuna uwezekano wa makadirio kutokuwa sahihi.
- Kuna uwezekano wa kuwepo kwa lengo batili la kughushi ambalo ni kosa la jinai kisheria.
- Kupoteza fedha zako.
- Ukipatikana na nyaraka ya kughushi utashitakiwa kwenye vyombo vya dola na kupata usumbufu ambao ungeweza kuuepuka.

7. Kipindi cha malipo ni lini?

Kodi ya ardhi hulipwa mwaka wa fedha wa Serikali unaoanzia tarehe 1 Julai. Baada ya tarehe 31, Desemba ya kila mwaka kodi hiyo hulipwa pamoja na tozo la adhabu.

8. Kama kodi hulipwa katika mwaka wa fedha, kwa nini baada ya Desemba kuna adhabu (penalty)?

Kulingana na Mkataba, malipo ya kodi ya pango la ardhi yanatakiwa kufanywa kila mwaka tarehe 1 Julai ndani ya muda wa siku 30. Kwa hali halisi, kuna ugumu wa watu wote kulipa ndani ya muda huo. Kutokana na hilo,

Sheria Na.4 ya mwaka 1999 sehemu ya 33 aya ya 11 imetoa mwanya kwa walipa kodi kuendelea kulipa bila adhabu hadi tarehe 31 Desemba ya mwaka unaohusika. Baada ya hapo adhabu inatozwa.

9. Kumbukumbu gani muhimu zinahitajika wakati wa malipo?

Kwa wale ambao kumbukumbu zao za umiliki zilishaingizwa kwenye Kompyuta wanatakiwa wakumbuke namba ya kumbukumbu ya kulipia yenye tarakimu sita (Lot Id Number).

Wengine wote wafike na risiti/ staka-badhi ya mwisho ya malipo na nakala ya hati au barua ya toleo(Original Letter of Offer).

Malipo ya kodi kwa toleo jipya la Kiwanja(Letter of Offer) yalipwe ndani ya muda wa siku 30 kuanzia tarehe ya toleo vinginevyo, itachukuliwa kwamba umekikataa kiwanja ulichopewa.

10. Nini athari ya kutolipa kodi ya ardhi?

- Kushitakiwa mahakamani kwa kutolipa kodi ya Serikali kulingana na Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 sehemu ya 50.
- Kushikwa na kuuzwa mali yako kwa kutumia madalali kulingana na sheria.



- Kufutiwa miliki ya ardhi kulingana na Sheria ya ardhi Na.4 ya mwaka 1999 sehemu 49-51.

11. Malipo kwa njia ya Hundi

Malipo yote yatakayofanywa kwa kutumia hundi, yaandikwe kwa:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya
Makazi,
S.L.P 9132
Dar es Salaam.